

Machukizo au Chukizo ni nini? kama tunavyosoma katika biblia?

---

**Machukizo** linatokana na neno “**chukizo**” na chukizo ni kitu kinachosababisha **chuki/hasira**. Kwa Mungu kitu chochote kinachoipandisha ghadhabu yake kinaitwa “chukizo”.

Na vitu vifuatavyo ndivyo vilivyokuwa machukizo kwa MUNGU.

### **1. Ibada ya Sanamu.**

Sanamu ya aina yoyote ile ilikuwa ni machukizo kwa Mungu na hicho ndicho kitu cha kwanza kilichokuwa kinaletea wivu kwa Mungu.

*Kumbukumbu 27:15 “Na alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya kuchonga, au ya kusubu, machukizo kwa Bwana, kazi ya mikono ya fundi, akaisimamisha kwa siri. Na watu wote wajibu, waseme, Amina”.*

*Kumbukumbu 32:16 “Wakamtia wivu kwa miungu migeni,  
Wakamkasirisha kwa machukizo.*

*17 Walitoa sadaka kwa pepo, si Mungu, Kwa miungu wasiyojua,  
Kwa miungu mipya iliyotokea siku zilizo karibu, Ambayo baba zenu  
hawakuilogopa”.*

Soma pia ***Kumbukumbu 27:15, na 2Wafalme 23:24***

## **2. Uasherati na ulawiti.**

*Walawi 18: 22 “Usilale na mwanamume mfano wa kulala na  
mwanamke; ni machukizo”.*

Soma tena *Mambo ya Walawi 20:13*

## **3. Mavazi yasiyopasa.**

*Kumbukumbu 22:5 “Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako”*

Mfano wa mavazi yasiyopasa, ni suruali kwa mwanamke, na nguo mfano wa magauni kwa wanaume.

#### **4. Sadaka yenye kasoro.**

*Kumbukumbu 23:18 “Usilete ujira wa kahaba, wala mshahara wa mbwa, katika nyumba ya Bwana, Mungu wako, kwa ajili ya nadhiri yo yote; kwani haya ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako, yote mawili”.*

*Kumbukumbu 17:1 “Usimchinjie Bwana, Mungu wako, ng’ombe wala kondoo aliye na kilema, wala neno ovu lo lote; kwa kuwa hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako”.*

## **Na yapo machukizo mengine mengi!.**

Lakini pia lipo chukizo moja **KUU na KUBWA** ambalo litatokea kule YERUSALEMU, ambalo ni **CHUKIZO LA UHARIBIFU**, linalomhusu Mpinga-kristo.

Kwa upana juu ya CHUKIZO LA UHARIBIFU, basi fungua hapa  
>>**CHUKIZO LA UHARIBIFU**

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:  
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

**Mafundisho mengine:**

**MAVAZI YA NDANI NA YA NJE.**

**VIPIMO MBALIMBALI VYA KIBIBLIA.**

**Kemoshi ni nani? (Yeremia 48:46)**

**Kwanini kuwe na kitabu Cha kumbukumbu la Torati na kwanini  
kiitwe vile?**

**Je! Shetani anao uwezo wa kuumba, kama Mungu?**

**Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp